

## Maziwa ya Wahisani

### Je, mbona maziwa ya mama ni muhimu sana kwa mtoto wangu?

Maziwa ya mama mwenyewe ndiyo chakula bora zaidi kwa mtoto wako mchanga. Maziwa ya mama mwenyewe huzalishwa nawe kwa njia ya kipekee kwa ajili ya mtoto wako. Kuna kingamwili na protini, kabohaidreti na mafuta maalum ambayo husaidia kuwezesha uwezo wa mtoto wako wa kupambana na maambukizi.

Watoa huduma wa afya wa mtoto wako wanakuhimiza kukama kwa pampu maziwa kutoka kwenye matiti yako ndani ya saa 1-2 za kwanza baada ya kujifungua. Maziwa yako ya mama ndiyo chakula muhimu zaidi ambacho mtoto wako anaweza kupokea. Wakati mwingine, kina mama hupata ugumu kuzalisha maziwa ambayo mtoto wako anahitaji. Mtoa huduma wako wa afya anaweza kuzungumza nawe kuhusu matumizi ya maziwa yanayoitwa Maziwa ya Binadamu ya Wahisani.

### Je, maziwa ya binadamu ya wahisani ni nini?

Maziwa ya wahisani ni *maziwa ya binadamu* ambayo hutayarishwa kwa kupashwa joto ili kuyafanya salama kutumika. Maziwa hayo yametolewa kama mchango na kina mama ambao walikuwa na maziwa mengi kuliko kiasi ambacho mtoto wao alihitaji au labda walifiwa mtoto wao na wakaamua kutoa mchango ili kumkumbuka mtoto wao. Kila mama hufanyiwa uchunguzi kwa makini, kwa mazungumzo na kimatibabu, kabla ya maziwa ya mama yaliyotolewa kama mchango kukubaliwa.

### Je, mbona utumie maziwa ya binadamu ya wahisani?

Wakati mwingine, kwa sababu za afya au za kihomoni, maziwa ya mama hucheleva kuzalishwa au kiasi kinachozalishwa na mama kinaweza kuwa kidogo. Maziwa ya wahisani ni rahisi kwa mtoto kumeng'anya kuliko fomula. Maziwa ya binadamu ya wahisani pamoja na maziwa ya mama mwenyewe pia yameonekana kusaidia kupunguza hatari ya kupata maradhi mabaya ya tumbo yanayoitwa *necrotizing enterocolitis*. Ugonjwa huu unaweza kumfanya mtoto wako kuwa mgonjwa sana. Mtoa huduma wa afya wa mtoto wako atazungumza nawe kuhusu matumizi ya maziwa ya mama ya wahisani kwa mtoto wako ikiwa inahitajika.

### Je, maziwa ya wahisani ni salama?

Kina mama wote wahisani hufanyiwa uchunguzi kwa makini. Kina mama wahisani lazima wawe na afya njema na kuwa hawatumii dawa. Pia huombwa kufanyiwa tathmini ya kimatibabu ya damu kabla ya kutoa mchango wa maziwa yao ya mama. Huwa wanatuma maziwa yao ya mama kwenye hifadhi ya maziwa ambako hukusanywa pamoja na kutayarishwa kwa kupashwa joto. Maziwa hayo hupimwa ili kuhakikisha hayana viini vya maradhi, na kisha kugandishwa. Kontena hizi zilizogandishwa hutumwa kwenye Kitengo cha Uangalizi Makini wa Watoto Wachanga (Neonatal Intensive Care Unit, NICU) na kuhifadhiwa zikiwa zimegandishwa hadi zinapohitaji kutumika.

Maelezo haya hayachukui nafasi ya ushauri wa mtoa huduma wako wa matibabu, mpango wa tiba, au elimu inayotolewa na muuguzi au mtoa huduma wako mwingine.

Hakikisha unafuata mpango wako binafsi wa huduma. Hakuna chochote kwenye makala haya kinachochukuliwa kuwa ushauri wa kimatibabu, uchunguzi wa kubainisha tatizo au tiba. Ikiwa una maswali kuhusu maelezo haya au mengine yoyote ya kimatibabu, zungumza na mtoa huduma wako. Omba usaidizi mara moja ikiwa unahitaji huduma za matibabu ya dharura.

Ikiwa uko nje ya hospitali, piga simu kwa 911. Ikiwa wewe ni mgonjwa hospitalini, omba usaidizi kutoka kwa muuguzi wako au mhudumu mwingine yeyote wa timu yako ya huduma.



## Una maswali?

Muulize mhudumu wa timu ya huduma za afya ya mtoto wako ikiwa una maswali zaidi. Pia unaweza kupata habari zaidi kuhusu maziwa ya wahisani kupitia tovuti hizi:

- Muungano wa Kuhifadhi Maziwa ya Binadamu wa Marekeni Kaskazini (Human Milk Banking Association of North America, HMBNA) – Tembelea [www.hmbana.org](http://www.hmbana.org)
- Ohio Health Mothers Milk Bank (Hifadhi ya Maziwa ya Mama ya Ohio Health) – Tembelea <https://www.ohiohealth.com/locations/womens-health/mothers-milk-bank/>

9/2023

Maelezo haya hayachukui nafasi ya ushauri wa mtoa huduma wako wa matibabu, mpango wa tiba, au elimu inayotolewa na muuguzi au mtoa huduma wako mwingine.

Hakikisha unafuata mpango wako binafsi wa huduma. Hakuna chochote kwenye makala haya kinachochukuliwa kuwa ushauri wa kimatibabu, uchunguzi wa kubainisha tatizo au tiba. Ikiwa una maswali kuhusu maelezo haya au mengine yoyote ya kimatibabu, zungumza na mtoa huduma wako. Omba usaidizi mara moja ikiwa unahitaji huduma za matibabu ya dharura.

Ikiwa uko nje ya hospitali, piga simu kwa 911. Ikiwa wewe ni mgonjwa hospitalini, omba usaidizi kutoka kwa muuguzi wako au mhudumu mwingine yeyote wa timu yako ya huduma.



Muulize mfanyakazi kuhusu wakalimani na huduma na misaada mingine ya ufikiaji wa lugha, inayopatikana bila malipo kwa wagonjwa na familia.  
Pregunte a un miembro del personal acerca de los intérpretes y otros servicios y ayuda para el acceso al idioma que están a su disponibilidad sin costo alguno.

